**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO**

**<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>**

**<u>MKUTANO WA NNE</u>**

**<u>Kikao cha Pili – Tarehe 09 Septemba, 2021.</u>**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

**<u>Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:</u>**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na kuweka masharti bora ndani yake.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:</u>**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na kuweka masharti bora ndani yake.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

58. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kikao cha Bajeti, Serikali iliulizwa kuhusu kufungwa kwa vituo vidogo vidogo vya Polisi (Police Post) katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Serikali ilikiri kwamba ni kweli vituo hivyo vimefungwa kutokana na ukosefu wa askari Polisi wa kutosha.

(a) Kwa kuwa vituo hivyo vingi vinasaidia sana wananchi katika maeneo hayo na kwa kuwa kufungwa kwake kumesababisha wimbi la uhalifu kuongezeka. Je, Serikali haioni haja kwamba wakati umefika kwa SMZ na SMT kuzungumza ili vijana wa JKU wanaojenga taifa kuchanganywa na Polisi kulinda vituo hivyo.

(b) Je, vijana wangapi wa kujitolea hujiunga na JKU kwa kila mkupuo.

110. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali inastahiki pongezi kwa kuanzisha na kwa nia yake ya kutaka kuuboresha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF). Hata hivyo, kwa kuwa madhumuni makuu ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ni kuleta uwiano wa maendeleo katika majimbo na kwa kuwa majimbo ya mjini na vijijini yametafautiana kwa vipaumbele na mahitaji ya maendeleo.

(a) Je, Serikali inatumia vigezo gani tofauti kwa kila jimbo katika kutoa ruzuku ya Mfuko huo.

(b) Je, kiwango cha sasa cha shilingi milioni 20 kimezingatia vigezo gani katika uhalisia wa utekelezaji wa madhumuni yake.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

120. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imekuwa mara kwa mara ikitoa na kufadhili mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, kwa kuzingatia dhana ya utawala bora, kuwepo kwa mgongano wa maslahi na kwa kutambua kwamba moja ya majukumu ya Baraza la Wawakilishi ni kujadili bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuiruhusu Ofisi ya CAG kuendelea kuendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kutetea ripoti zilizoandikwa na CAG ni kinyume na takwa la utekelezaji wa utawala bora.

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kulilazimisha na kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kutafuta wakufunzi na wawezeshaji wa kujitegemea wasiokuwa Ofisi ya CAG kuwapatia mafunzo juu ya kuzichambua ripoti zilizoandikwa na Ofisi ya CAG.

(c) Je, ni Sheria ipi iliyo halali inayolazimisha au kupendekeza Ofisi ya CAG kuwapa mafunzo juu ya kuzichambua ripoti zilizoandikwa na CAG.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

80. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka, kuna uandaaji wa ripoti za pamoja (Consolidation Report) na ripoti za ufafanuzi (Segment Report). Kwa kuwa taasisi zetu zipo Unguja na Pemba.

Je, kwa nini taasisi za Serikali zilizopo Pemba zisifunge hesabu zake za mwaka (Segment Report).

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

147. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Jimbo la Kiembesamaki ni miongoni mwa majimbo yaliyobarikiwa na wawekezaji wa sekta tofauti. Hata hivyo, jimbo hili linakabiliwa na tatizo la ajira ambazo zinakosesha mahusiano mema ya jamii na wawekezaji hao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Kiembesamaki kupata ajira na kujenga mahusiano mema katika jimbo hilo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

38. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwenye miaka ya thamanini (80) na tisini (90), riadha ilikuwa ni moja kati ya mchezo ulioipatia sifa kubwa Zanzibar kwenye mashindano mbali mbali ya ndani na nje ya nchi, na hatimae kuweza kupata medali za kitaifa na kimataifa, jambo ambalo lilipelekea Serikali kumuajiri kocha wa kimataifa wa mchezo huo Tambwelea kutoka Cameroon.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea mchezo huu adhimu kupoteza umaarufu na hatimae kupotea kabisa hapa Zanzibar.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

1. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika hali ya kukua kwa uchumi hapa nchini, miji mbali mbali imezidi kuongezeka na kufanya miundombinu ya barabara na madaraja kuzidiwa na wakaazi wa maeneo hayo. Katika kijiji cha Maziwani Shengejuu, kumekuwa na daraja dogo ambalo hukatisha maisha ya watu kila kipindi cha mvua kinapoanza.

(a) Je, Serikali imekwama wapi katika jitihada za kuwatengezea wananchi daraja hilo.

(b) Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Jimbo la Pandani kuhusu ujenzi wa daraja hilo kwa kuwa imekuwa imeahidi kufanya hivyo zaidi ya miaka 48 kwa sasa.

5. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein aliahidi kuwekwa taa za barabarani katika barabara ya Fuoni kuanzia kwenye daraja la Dkt. Shein hadi kituo cha Polisi Fuoni.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

63. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Pamoja na kuwa Zanzibar tumejaaliwa bahari yenye samaki wengi, bado kuna tatizo la ongezeko la uvuvi haramu.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani katika hatua za kuzuia vitendo vya uvuvi haramu.

(b) Kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu ni kwa kiasi gani mamlaka husika zinawajibika.

(c) Je, Serikali imeshawahi kutoa elimu ya uvuvi haramu kwa wavuvi wetu.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

34. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mfumo wa elimu uliopo hivi sasa visiwani Zanzibar unapelekea watoto kuanza skuli wakiwa na umri wa miaka sita, hali inayowapelekea watoto hawa kumaliza masomo yao ya Sekondari wakiwa na umri wa miaka kumi na tano (15).

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwasaidia wanafunzi ambao wanashindwa kuendelea na masomo yao ya kidato cha tatu.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha mfumo wa utoaji wa elimu ya msingi hadi darasa la saba kwa lengo la kuwajengea watoto wetu mustakbali mwema wa maisha yao ya baadae.

114. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa nia njema, Serikali ilifanya mageuzi ya elimu na kuifanya skuli ya msingi kuwa ya miaka sita badala ya saba au nane kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Hata hivyo, kumekuwa na manung'uniko mengi kuulalamikia mfumo huo wa miaka sita ya skuli ya msingi Zanzibar wakati Tanzania Bara wakiwa na miaka saba ya skuli ya msingi.

(a) Je, ni ipi tathmini ya Serikali kuhusu kufanikiwa au kutokufanikiwa kwa mfumo mpya wa miaka sita ya skuli ya msingi.

(b) Kwa vile kumekuwa na mzigo mkubwa wa masomo katika mfumo huu wa miaka sita ya elimu ya msingi, Serikali haioni haja ya kurejea kwenye mfumo wa asili wa miaka saba au nane ya elimu ya msingi sambamba na kupunguza idadi ya masomo kwa wanafunzi, kupunguza mzigo wa kazi za nyumbani na kuongeza madarasa ya kusomea.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

145. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wanafunzi wanaosoma chuo cha Afya cha Muhimbili (MUHAS) wanaotoka Wizara ya Afya Zanzibar kucheleweshewa posho za kujikimu kwa mwaka wa masomo 2020/2021 huku hali yao ya maisha ikiwa ngumu na gharama za mahitaji yao kuwa kubwa.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani kusawazisha hali hiyo.

(b) Kwa vile wanafunzi hawa wameshaandika barua Wizarani muda mrefu bila ya kupewa mrejesho, Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia posho zao kwa haraka.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

88. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunaishukuru sana Serikali kwa kuliruhusu Shirika letu la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) kuanzisha jengo lake kisiwani Pemba, katika Jimbo la Chake Chake. Kukamilika kwa jengo hilo, kungelisaidia sana kuimarisha huduma za Shirika hili na kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma hizo kwa urahisi. Hata hivyo, jengo hilo lililokusudiwa kujengwa limekwama katika hatua za awali kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, kuna sababu zipi za msingi zilizopelekea jengo hilo kukwama tokea lilipoanza kujengwa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikamilisha jengo hilo ili liweze kutoa huduma zilizokusudiwa.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

96. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika eneo la Mtemani Wete mkabala na ukumbi wa Baraza la Wawakilishi mwelekeo wa barabara ya Konde, kuna jengo ambalo upande mmoja unamilikiwa na mtu binafsi na upande wa pili unamilikiwa na Serikali. Kwa kuwa jengo hilo lilijengwa wakati mmoja likiwa na wamiliki wawili tofauti na kwa kuwa nyumba inayomilikiwa na mtu binafsi iko imara, na nyumba ya Serikali ni mbovu na imekuwa kama gofu ambalo linahatarisha maisha ya wakaazi wa eneo hilo.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kulieleza Baraza hili tukufu kwamba, ni sababu zipi zilizopelekea nyumba hii ya Serikali kuwa katika hali hiyo.

(b) Je, ni kwanini Serikali inashindwa na mtu binafsi katika kuitunza nyumba hii.

(c) Je, ni lini Wizara imepanga kuifanyia marekebisho nyumba hii pamoja na nyumba nyengine za Serikali zenye sura kama hii ili kunusuru maisha ya raia wetu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Kuweka Usimamizi mzuri wa Shughuli za Kiislam Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na kuweka masharti bora ndani yake – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**09 Septemba, 2021.** **KATIBU WA BARAZA.**